TANGAZO LA SERIKALI NA. 4 LIMETOLEWA TAREHE 4/1/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA. NA 272)

_____

AMRI

_____

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))

_____

AMRI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA ("BUKOBA WSSA") (YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba ("Bukoba WSSA")(ya Kurekebisha Bei za Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2018.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Januari 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Bukoba WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 31 Machi 2019 au kabla, Bukoba WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa

masharti ya Amri hii;

(b) Bukoba WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(c) Bukoba WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(d) Bukoba WSSA itazingatia kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA, Sura. 414 na Kanuni za EWURA (Fees and Levies Collection Procedure), GN. Na.193 ya Mwaka 2010;

(e) Bukoba WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(f) Bukoba WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Bukoba WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Bukoba WSSA katika siku zijazo.

Kutenguliwa kwa

5. Amri hii inatengua matumizi ya Amri Na. 2016-

Amri

002 ya tarehe 1 Februari 2016 ya bei za maji zinazotozwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Bukoba WSSA).

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Makundi ya Wateja	Bei za Sasa		Bei Zilizoidhinishwa		
	Matumizi (mita za Ujazo)	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	0-5	1,345	1,570	1,840	2,150
	>5-10	1,370	1,600	1,870	2,190
	Zaidi ya 10	1,395	1,630	1,910	2,230
Taasisi	0-5	1,500	1,800	2,100	2,540
	>5-10	1,545			
	Zaidi ya10	1,620			
Biashara	0-5	1,510	1,860	2,200	3,000
	>5-10	1,555			
	Zaidi ya10	1,640			
Viwanda	0-5	1,810	2,200	2,600	3,000
	>5-10	1,845			
	Zaidi ya10	1,915			
Magati		750	1,500	1,500	1,500
BEI YA WASTANI			**1,613**	**1,888**	**2,206**

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

Makundi ya Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	3,000	Tozo ya Huduma imeondolewa		

Taasisi	4,500	
Biashara	5,000	
Viwanda	5,000	

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Makundi ya Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Wateja Wote	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013		

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Makundi ya Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	10,000	10,000	10,000	10,000
Taasisi	20,000	20,000	20,000	20,000
Biashara	30,000	30,000	30,000	30,000
Viwanda	60,000	60,000	60,000	60,000

Jedwali Namba 1(e): Tozo ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Uondoaji wa Majitaka (Shilingi/Tripu)

Makundi ya Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Wateja Wote	100,000	150, 000	150,000	150,000

Jedwali Namba 1(f): Tozo ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Umwagaji wa Majitaka (Shilingi/Tripu)

Makundi ya Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Magari ya Aina Zote	7,000	7,000	7,000	7,000

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA - MILIONI SHILINGI

Maelezo ya Kazi zitakazofanyika				Jumla
	2018/19	2019/20	2020/21	
Ukarabati na Mabadilisho ya Miundombinu				
Matengenzo makubwa ya mtambo wa kutibu maji kama vile kubadilisha nozzles, chujio.	62.9	45.9	-	109
Kununua VFD (variable speed drives), mpya, Impellers and shafts kwa ajili ya pampu za kuzalisha maji.	25.0	45.0	65.0	135
Jumla Ndogo (Ukarabati na Mabadilisho)	**88**	**91**	**65**	**244**
Miradi Mipya				
Kuweka mabomba ya kusafirisha na kusambaza maji ya aina ya PVC and HDPE yenye kipenyo cha 50mm mpaka 250mm ili kuhudumia maeneo ya Kata za Nshambya, Buhembe, Nyanga, sehemu ya Kahororo na Kalabagaine. Jumla ya mabomba ya km 109 yatalazwa.	45.0	45.0	45.0	135
Kujenga nyumba ya kusukumua maji na kuweka pampu za kuongeza msukumo wa maji katika maeneo ya Machichioni, Nsambya and	61.9	66.0	60.3	188

Tangazo la Serikali Na. 4 (linaendelea)

Maelezo ya Kazi zitakazofanyika				**Jumla**
	2018/19	**2019/20**	**2020/21**	
Itahwa				
Kununua dira za wateja 8,000	120.0	85.0	127.5	333
Kujenga nyumba wa wahudumu	-	25.0	35.0	60
Kununua samani mpya kwa ajili ya kubadilisha zilizochakaa.	5.0	5.0	5.0	15
Kununua compyuta na vifaa vyake kwa ajili ya kubadilisha zilizochakaa.	25.0	20.0	35.0	80
Jumla Ndogo (Miradi Mipya)	**257**	**246**	**308**	**811**
Jumla Kuu ya Gharama za Uwekezaji	**345**	**337**	**373**	**1,054**

JEDWALI LA TATU

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

Maelezo	**Uniti**	**Lengo la Utendaji**		
		2018/19	**2019/20**	**2020/21**
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	Na	775	1,451	1,240
Kiwango cha upotevu wa maji	**%**	40	35	30
Wateja wenye Dira	%	100	100	100
Wastani wa Masaa ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji kwa Mteja	Masaa	24	24	24

Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	95	95	95

Dodoma,
....., 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu